TANGAZO LA SERIKALI Na. 933 La Tarehe 23/10/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO ZA HIFADHI YA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Mji wa Korogwe za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo-

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Korogwe;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote;

"maeneo ya malisho" maana yake ni sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Kijiji kuwa maeneo ya malisho ya mifugo;

Sura ya 191

"mazingira" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

Sura ya 323

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia kumi ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia hamsini au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo imetangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri.

Masharti kuhusu ufugaji

3.-(1) Mtu yeyote anayefuga katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;

(b) kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(c) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(d) kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(e) kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(g) kuweka alama kwenye mifugo yake na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;

(h) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(i) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri; na

(j) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:

(a) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(b) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;

(c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(e) kufuga mifugo kwa zaidi ya idadi iliyoelekezwa na Halmashauri; au

(f) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata mifugo inayokutwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kuchunga, kulisha au kunywesha mifugo.

(4) Endapo mmiliki wa mifugo iliyokamatwa kwa mujibu wa aya ya (c) ya kifungu kidogo cha (2) na kifungu kidogo cha (3) atashindwa kulipa faini kama ilivyoanishwa katika Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza, baada ya kupata amri ya Mahakama, kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mifugo hiyo na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo baada ya kutoa gharama za ukamataji, utunzaji wa mifugo na Mahakama.

Masharti kuhusu kilimo

4.-(1) Mtu yeyote anayelima katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) taratibu za kilimo kwa kuzingatia kalenda ya

kilimo ya Halmashauri na kwa kuzingatia Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi na mazingira;

(b) kutolima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) kutotumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(d) kutosafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto, isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Kibali cha kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa nne kamili asubuhi na saa kumi na mbili jioni hadi saa moja kamili usiku.

(4) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:

(a) kutozingatia kalenda ya kilimo ya Halmashauri;

(b) kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, milima, mabwana au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) Kutumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; au

(d) kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto bila ya kuwa na kibali au nje ya muda ulioruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

5.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchimba mchanga, kokoto, mawe, udongo au madini yoyote ya ujenzi kwa madhumuni ya kibiashara karibu na makazi ya watu, maeneo ya hifadhi, kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(3) Mtu yeyote anayetaka kuchimba mchanga, kokoto au mawe katika eneo la Halmashauri atatuma maombi yake kwa njia ya maandishi na kulipia ada ya maombi hayo kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo za Halmashauri zilizotungwa mahsusi kwa ajili ya kuainisha ada na ushuru unaotozwa na Halmashauri.

Uhifadhi wa vyanzo vya maji

6.-(1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa-

(a) kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Halmashauri;
(b) kutoishi katika eneo la hifadhi au chanzo cha maji;
(c) kutolima, kutokata miti, kutochunga mifugo au kutofanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote eneo lililotangazwa kuwa eneo la hifadhi au chanzo cha maji;
(d) kutoelekeza mabomba ya maji machafu au kujisaidia kwenye mito, mabwawa, maziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji; au
(e) kujimilikisha eneo ambalo ni chanzo cha maji cha umma.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa misitu

7.-(1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa:

(a) kutokata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri;

(b) kutochoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika eneo la Halmashauri;

(c) kutovuna miti isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri; au

(d) kutovuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe malumu.

(2) Uchomaji wa mkaa utafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri katika maeneo yaliyotengwa mahsusi kwa ajili hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Utupaji wa taka

8.-(1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kuwa na shimo au chombo maalumu cha kuhifadhi taka ngumu na laini na gharama za utupaji wa taka hizo kwenye jaa la taka ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwa na choo safi na salama.

(2) Halmashauri itatakiwa kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo hilo.

(3) Vikundi vya kijamii vitakavyokuwa vimeundwa kwaajili ya kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye dampo vitakusanya ada za uzoaji wa taka ngumu kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa viwanda

9.-(1) Mtu yeyote hatoruhusiwa kuendesha shughuli za kiwanda au karakana au shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

(2) Mtu yeyote hatoruhusiwa, bila sababu za msingi, kufanya matengenezo ya magari, pikipiki au mitambo katika eneo lolote isipokuwa katika karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali na kulipa ada kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo mahsusi kwa ajili ya ada na ushuru unaotozwa na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa jumla

10.-(1) Wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira yameharibiwa watakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida eneo hilo kwa kupanda miti na kuendelea kutoharibu mazingira ili kuwezesha uoto au mazingira yarudi katika hali yake ya kawaida kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(2) Wakazi wa eneo ambalo moto umetokea unaotishia maisha ya watu, mali au mazingira watakuwa na wajibu wa kushiriki kuzima moto huo kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Kila Halmashauri ya Serikali ya Kijiji itatakiwa kutenga eneo la hifadhi ya misitu, kusimamia kila mwanakijiji anapanda miti isiyopungua kumi katika eneo la makazi na miti hamsini katika eneo la shamba, kila shule au taasisi ya umma inapanda miti ya kukinga upepo kuzunga majengo.

(4) Mtu yeyote atakayeshindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza maelekezo ya Halmashauri chini ya kifungu kidogo cha (1), (2) na cha (3) atakuwa ametenda kosa.

Ukaguzi

11. Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa atakua na uwezo wa kuingia katika muda wa kazi, katika eneo lolote kwa madhumuni ya kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi, na ada ya ukaguzi italipwa mara moja kwa mwaka kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hizi atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufililisha kosa

13. Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa endapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa kumtoza kiasi cha shilingi elfu thelathini baada ya kujaza fomu maalumu iliyoambatishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) (a))*

GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA KWENYE JAA LA TAKA

| Na. | Kiasi cha taka | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Gari chini ya tani tano kwa safari | 40,000/= |
| 2. | Gari la tani tano na zaidi kwa kila tani moja inayoongezeka | 10,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (3))*

GHARAMA ZA UKUSANYAJI TAKA KATIKA MAJENGO YA BIASHARA NA MAKAZI

| NA. | AINA YA BIASHARA | VIWANGO |
|---|---|---|
| 1 | Makazi au kaya | 5000/= kwa mwezi |
| 2 | Mgahawa mkubwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 3 | Nyumba ya kulala wageni | 10,000 kwa mwezi |
| 4 | Zahanati (Taka zisizo hatari) | 10,000/= kwa mwezi |
| 5. | Kituo cha afya (taka zisizo hatari) | 15,000/= kwa mwezi |
| 6 | Hospitali | 30,000/= kwa mwaezi |
| 7 | Kiwanda cha kuuza mbao | 30,000/=kwa mwezi |
| 8. | Fundi seremala | 5000/= kwa mwezi |
| 9. | Fundi chuma | 5000/=kwa mwezi |
| 10 | Karakana | 20,000/=Kwa mwezi |
| 11 | Kiwanda kidogo | 20,000/= kwa mwezi |
| 12 | Kiwanda kikubwa | 20,000/=kwa mwezi |
| 13. | Duka la jumla | 20,000/=kwa mwezi |
| 14. | Duka la rejareja au huduma | 3000/= kwa mwezi |
| 15. | Shule ya msingi ya bweni (binafsi) | 20,000/=kwa mwezi |
| 16. | Shule ya msingi ya kutwa (binafsi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 17. | Shule ya sekondari ya kutwa (binafsi) | 15,000/=kwa mwezi |
| 18. | Shule ya sekondari ya bweni (binafsi) | 30,000/=kwa mwezi |
| 19. | Duka dogo la chakula (min supermarket) | 5000/=kwa mwezi |
| 20. | Duka kubwa la chakula (supermarket) | 10,000/= kwa mwezi |
| 21. | Baa | 10,000/= kwa mwezi |
| 22. | Kilabu ya usiku | 20,000/= kwa mwezi |
| 23. | Kambi ya sherehe | 30,000/=kwa mwezi |
| 24. | Duka la kuuza nyama na samaki | 10,000/=kwa mwezi |
| 25. | Duka la dawa (jumla na Rejareja) | 10,000/=kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 26. | Duka la dawa (Rejareja) | 5,000/=kwa mwezi |
| 27. | Kiwanda kidogo kwa trip zisizozidi 4 kwa mwezi | 50,000/=kwa mwezi |
| 28. | Dobi mdogo | 1,000/=kwa mwezi |
| 29. | Dobi mkubwa | 5,000/= kwa mwezi |
| 30. | Fundi wa vifaaa vya umeme | 5,000/=kwa mwezi |
| 31. | Fundi kushona kwa kila sherahani | 1,000/=kwa mwezi |
| 32. | Saluni | 5,000/=kwa mwezi |
| 33. | Kituo cha kuuza mafuta | 50,000/=kwa mwezi |
| 34. | Stoo | 5,000/=kwa mwezi |
| 35. | Ghala | 30,000/=kwa mwezi |
| 36. | Hoteli ( ya kitalii) | 100,000/=kwa mwezi |
| 37. | Hoteli (ya kawaida) | 50,000/=kwa mwezi |
| 38. | Taasisi | 100,000/=kwa mwezi |
| 39. | Klabu ya pombe ya asili | 10,000/=kwa mwezi |
| 40. | Kituo cha michezo | 5,000/=kwa mwezi |
| 41. | Dahalia (hostel) | 10,000/=kwa mwezi |
| 42. | Uwanja wa michezo | 20,000/=kwa mwezi |
| 43. | Stoo za mkaa | 10,000/=kwa mwezi |
| 44. | Mama lishe au baba lishe. | 1,000/=kwa mwezi |
| 45. | Duka la kuuza magari | 50,000/=kwa mwezi |
| 46. | Vituo vya kuoshea magari | 20,000/=kwa mwezi |
| 47. | Aina nyingine ya biashara au huduma | 10,000/=kwa mwezi |

JEDWALI LA TATU

*( Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

GHARAMA ZA UKAGUZI

| NA. | ENEO AU JENGO | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1. | Viwanda vikubwa | 180,000/=kwa mwaka |
| 2. | Viwanda vidogo | 60,000/=kwa mwaka |
| 3. | Hoteli za kitalii | 180,000/= kwa mwaka |
| 4. | Hoteli za kawaida | 120,000/=kwa mwaka |
| 5. | Migahawa | 60,000/=kwa mwaka |
| 6. | Baa | 60,000/=kwa mwaka |
| 7. | Nyumba za kulala wageni | 120,000/=kwa mwaka |
| 8. | Maduka ya Rejareja | 60,000/= kwa mwaka |
| 9. | Maduka ya jumla | 120,000/=kwa mwaka |
| 10 | Gereji | 60,000/=kwa mwaka |
| 11. | Maeneo ya kuosha magari | 60,000/=kwa mwaka |
| 12. | Wauza mbao au mabanzi au milunda | 120,000/=kwa mwaka |
| 13. | Taasisi | 120,000/=kwa mwaka |
| 14. | Supermakert | 120,000/= kwa mwaka |
| 15. | Magari yanayotembeza biashara | 60,000/=kwa mwaka |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 13)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ........................................................................ nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Mji wa Korogwe za Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ...................................................

Mbele ya:
Jina……................................................
Cheo: .................................................
Saini: .................................................
Tarehe: .............................................

Muhuri wa Halmashauri ya mji Korogwe ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 31/10/2019 Muhuri uliobandikwa mbele ya:-

NICODEMUS J. BEI,
*Mkurugenzi wa Mji,*
*Halmashauri ya Mji,*
*Korogwe*

MHE. HILLARY H. NGONYANI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Mji,*
*Korogwe*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
28 Septemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*